


# CRYSTAL® VC UTARATIBU WA HARAKA WA KIPIMO CHA UCHUNGUZI (RDT)




U.S. Department of  
Health and Human Services  
Centers for Disease  
Control and Prevention

## MUHIMU: Valia mavazi binafsi yanayofaa ya kujikinga unapofanya kipimo hiki.

1. Bandika kwenye neli ya kupima ya ml 5 kibandiko cha kumtambua mgonjwa. Weka kando.
2. Hakikisha chupa yenyé kitendanishi haijafunguliwa na mchanganyiko si mchafu au haujabadilika rangi. Tupa chupa ikiwa hairidhishi.
3. Fungua kichupa cha kutayarishia sampuli kisha ongeza sampuli ndani.
  - a. Kwa kinyesi kigumu, kigumu kidogo au majimaji, tumia kijiti cha sampuli ili kukusanya kiasi kidogo cha kinyesi kutoka kwenye maeneo mawili au zaidi katika ile sampuli na kuingiza kwenye kichupa cha kutayarishia sampuli. **KUMBUKA:** "Dunga" "usichote" ili kuepuka kuokota dutu za uchafu ambazo zinaweza kuziba kichungi cha kijiti cha kuchovya kwenye sampuli.
  - b. Kwa kinyesi chenyé umajimaji, tumia kichukua umajimaji ili kumwaga matone 2 ya sampuli kwenye kichupa cha kutayarishia sampuli.
4. Kaza kifuniko cha kichupa cha kutayarishia sampuli na kuitingisha ili kuchanganya mchanganyiko.
5. Vunja mwisho wa nje wa kifuniko kutoka kwa kile kichupa cha kutayarishia sampuli.
6. Gawa matone 4 ya sampuli iliyotayarishwa kwenye neli ya kupima ya mililita 5.
  
7. Kwa uangalifu fungua kifuko cha aluminu kwenye mstari ulio na matundu.
8. Kagua yaliyomo. **KUMBUSHO:** Gusa sehemu ya juu tu ya kijiti cha kuchovya sampuli.
  - a. Chunguza ikiwa kijiti cha kuchovya sampuli kimeharibika (k.m, hakina mipasuko, migawanyiko, kugeuza rangi).
  - b. Hakikisha kifuko kina kikausho ambacho hakijabadika kuwa rangi nyeupe.
  - c. Tupa kijiti cha kuchovya sampuli ikiwa kimeharibika, au ikiwa kikausho kinakosekana au kubadilika na kuwa rangi nyeupe.
9. Bandika kibandiko cha kumtambua mgonjwa kwenye sehemu ya juu ya kijiti cha kuchovya sampuli.
10. Weka kijiti cha kuchovya sampuli ndani ya neli ya kupima na alama ya mishale ikiwa inaangalia CHINI.
11. Thibitisha kuwa mwisho wa kile kijiti cha kuchovya sampuli ("sehemu ya kuchovya") kimezamishwa ndani ya sampuli iliyotayarishwa. **KUMBUKA: Alama ya mishale inapaswa kuwa juu ya kiwango cha sampuli.**
12. Subiri dakika 15-30, ondoa kijiti cha kuchovya sampuli na usome matokeo. (Angalia jedwali hapo chini kwa tafsiri ya matokeo.)
13. Weka taka zote katika mfuko wa plastiki yenyé matabaka mawili yaliyobandikwa kibandiko cha "Hatari kwa mazingira."



## Mtazamo wa Mchoro wa Kijiti cha kuchovya sampuli



## Tafsiri ya Matokeo

Tafsiri*	Mkanda wa rangi ya waridi-nyekundu umeonekana		
	O1	O139	Udhhibit
A. Vibrio cholerae O139 imeonekana	-	+	+
B. Vibrio cholerae O1 imeonekana	+	-	+
C. Vibrio cholerae O1 na O139 imeonekana	+	+	+
D. Vibrio cholerae O1 na O139 haijaonekana	-	-	+
E. Matokeo batili	+ au -	+ au -	-

\* Kanda ya udhibiti lazima itokee ili matokeo yachukuliwe kuwa ya halali.

## Mchoro wa Tafsiri ya Matokeo

